ADEN N. MWAKIPIKI

# 30 SECRET KEYS TO THE BEST

Mbinu 30 Rahisi Zitakazokufanya uwe
Bora katika kila eneo la maisha yako

# 30 SECRET KEYS TO THE BEST

## (FUNGUO 30 ZA SIRI YA KUWA BORA)

ADEN N. MWAKIPIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili au kudurufu sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi, kwani kufanya hivyo ni ukiukwaji wa haki za mwandishi. Ikigundulika hatua za kisheria zitachukuliwa.

Kusambaza au kuuza kitabu hiki bila idhini ya mwandishi ni kosa kisheria.

Copyright ©2021

Mawasiliano:

Aden N. Mwakipiki

Simu +255 713 315 452 / +255 755 851 971

Barua pepe: adenmwakipiki@gmail.com

SHUKRANI

Ninamshukuru sana Mungu kwa kuniwezesha kuandika na kukamilisha kitabu hiki, hivyo utukufu na heshima nampa yeye.

Ninakushukuru pia wewe mpendwa msomaji kwa utayari wako wa kusoma kitabu hiki.

**YALIYOMO**

Shukrani..... 4

Utangulizi..... 6

Mbinu 30 Rahisi zitakazokufanya uwe bora katika kila eneo la maisha yako..... 7

Kuhusu Mwandishi..... 92

Vitabu vingine vya Mwandishi..... 93

## UTANGULIZI

***“Nini SIRI ya mafanikio yako ?”*** hili ni swali au maneno ambayo kwa hakika si mageni kabisa katika ufahamu wako, ina wezekana umewahi kumuuliza mtu swali la namna hii, lakini pia inawezekana umewahi kuulizwa, au umewahi kusikia mtu akiuliza.

**SIRI**, ni ufunguo wa jambo fulani ambalo haliko wazi kiasi cha kila mtu kujua, na ili iwe siri lazima iwe ni jambo nyeti sana ambalo limefungwa (limefichwa), ambalo si watu wote wanaweza au wanapaswa kulijua isipokuwa kwa vigezo maalumu sana.

Ni ndoto na shauku ya kila mtu kufanikiwa na kuwa bora katika kila eneo la maisha yake, lakini kwa bahati mbaya ni kwamba mafanikio yoyote yale yamefichwa katika siri fulani ambayo wale wenye ufunguo wa siri hiyo ndio wanaoweza kuyafikia mafanikio hayo.

Kila mtu aliyefanikiwa katika maisha yake na kutambulika kwa mafanikio yake kuna siri anaijua ambayo kwayo aliweza kufikia hatua aliyofikia. Kila anaye endelea kufanya vizuri kila siku katika eneo lake la maisha, mfano katika

Sanaa, michezo, kazi, biashara, uongozi n.k basi ujue kuna siri anafahamu na anaendelea kuishi hiyo ndiyomaana anaendelea kuwa bora katika eneo hilo.

Siri kama ufunguo ni kanuni isiyo ya wazi ambayo mtu akiijua na kuiishi lazima atapata matokeo mazuri ya kile anachofanya. Mara zote kanuni inapofuatwa huleta matokeo ya kweli kulingana na muongozo wa kanuni hiyo, huwa haidanganyi.

Mtu akikaa katika siri lazima ataendelea kuwa bora na kufanikiwa sana, lakini akiacha kukaa na kuishi ile siri au kanuni lazima atapoteza mafanikio au nafasi yake.

**Kuwa Bora.** Ni kuwa katika nafasi nzuri ya kujikubali mwenyewe kwa matumizi ya kiwango cha juu ya uwezo wako na matokeo ya jitihada zako katika kila unachofanya.

Ni kuwa kwenye nafasi ya kwanza au nzuri zaidi katika machaguo ya watu wengine kwa kila unachofanya. Wakati unapofanya vitu vizuri zaidi kuliko wengine ndipo unapokuwa na nafasi nzuri ya kuwa bora ukilinganishwa na wengine wanaofanya vitu unavyofanya wewe.

Kuwa bora katika eneo fulani kwenye maisha si jambo jepesi na la wazi kiasi kwamba kila mtu anaweza kuwa hivyo, kuwa bora ni siri iliyofichika ambayo kila awezaye kuifichua anakuwa na nafasi ya yeye kuwa bora katika eneo hilo. Hivyo ukitaka kuwa bora lazima uzitambue siri za kuwa bora.

**Kuwa bora ni dhamana ya nafasi yako.**

Namna pekee itakayokufanya kuwa mtu wa pekee na usiyekuwa na mbadala katika chochote utakachokifanya ni wewe kuwa bora zaidi ya wengine.

*"Being The Best recommend you to be Irreplaceable in any position you're"*

Njia pekee na rahisi itakayokufanya uwe mtu asiye na mbadala katika kila eneo la maisha yako ni KUWA BORA katika kila kitu ufanyacho.

*"The only way to be irreplaceable in everything and everywhere you go is being the Best in everything you do"*

Dunia ya Sasa inakwenda kasi sana na mabadiliko yanatokeo kila siku kutokana na ukuaji wa sayansi na teknolojia.

Kutokana na mabadiliko hayo kumekuwepo na ushindani mwingi Sana katika kila kitu na kila nafasi ambayo mtu anaipata

Kwahiyo imekuwa vigumu sana mtu kupata nafasi katika kila eneo la maisha….

Lakini pia na vigumu zaidi kudumu katika nafasi hiyo pindi inapopatikana, wakati huo huo imekuwa rahisi sana kupoteza nafasi katika kila eneo la maisha ya watu kwa sababu ya ushindani kuwa mkubwa sana.

Namna pekee itakayoamua na kukufanya wewe upate nafasi katika ushindani ni kuwa bora zaidi ya wengine wote katika ushindani. Zaidi ni kwamba kitu pekee kitakufanya uendelee kubaki kwenye hiyo nafasi pia katika ushindani ni kuendelea kuwa bora zaidi kila siku.

Haikuwa rahisi kwa ***Daniel, Shadrak, Meshaki na Abednego kupewa nafasi katika ushindani wa maelfu***

***ya watu tena utumwani kama si viwango vyao vya ubora kuonekana viko juu mara kumi zaidi yaw engine***.

Kitu pekee kiliamua wao kushinda na kupata nafasi ni kiwango chao Cha UBORA kuwa kikubwa Mara kadhaa zaidi ya wale Wengine.

Kwahiyo UBORA Ni dhamana tosha ya nafasi yako katika kila eneo la maisha yako.

*“Being at your best guarantee your position in every aspect of your Life…”*

Mara baada ya kumaliza kusoma kitabu hiki utakuwa na uwezo wa *kujua funguo 30 za siri ya kuwa bora, namna ya kuishi funguo 30 za siri ya kuwa bora, na jinsi ya kubaki kwenye nafasi yako ya kuwa mtu bora katika kila eneo la maisha yako.*

Kuwa mtu yule ambaye watu wengine wanatamani kuwa kama wewe (*Be the person that other people want to be like)*

Ni shauku na imani yangu kwamba mara utakapomaliza kusoma na kuchukua hatua ya vitendo kwa kuyafanyia kazi yaliyo andikwa humu mara hutakuwa mtu wa kawaida.